



DISCOVERY NATIONAL EXAMINATIONS KCPE COMPLIANCE 2019

DARASA LA NANE



KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

Muda:Saa 1 dakika 40

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandikia chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lioneshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:
NAMBA YAKO YA MTHANI
JINA LAKO
JINA LA SHULE YAKO
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mthani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya majibu na usiikunje.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usikunje.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D.
Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lioneshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano

19. Tumia kiambishi sahihi:-
Darasa ___ tajengwa kesho.
A. i B. u C. li D. ki

Jibu sahihi ni C

Katika karatasi ya majibu

9 [A] [B] [C] [D] **19** [A] [B] [C] [D] **29** [A] [B] [C] [D] **39** [A] [B] [C] [D] **49** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 19, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Discovery Educational Publishers. Nairobi
Barua pepe:discoverypublishers@gmail.com

Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.

Discovery National Examinations 2019

GEUZA UKURASA

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Jaza kila pengo kwa jibu lifaalo.

Pana shughuli nyingine __1__ ambazo vijana wetu __2__ kujihusisha nazo __3__ kutumia dawa za kulevyia. Kwa mfano, kushiriki michezo mbalimbali __4__ kupata nguvu tu __5__ pia huwa chanzo cha kujipatia __6__. Ni __7__ la serikali yetu __8__ vijana kiasi fulani cha fedha ili __9__ wazitumie kujiimarisha. Vijana ndio viongozi wa siku za __10__.

- | | | | | |
|-----|-----------------|---------------|-----------------|-----------------|
| 1. | A. jingi | B. mingi | C. nyingi | D. mengi |
| 2. | A. wanaweza | B. wakiweza | C. wataweza | D. waliweza |
| 3. | A. baada ya | B. kabla ya | C. aghalabu | D. badala ya |
| 4. | A. hakuwasaidii | B. huwasaidia | C. kutawasaidia | D. kugewasaidia |
| 5. | A. mbali | B. ila | C. bali | D. isipokuwa |
| 6. | A. raha | B. riziki | C. umaskini | D. hasara |
| 7. | A. wajibu | B. jukumu | C. kazi | D. dhima |
| 8. | A. kutenga | B. kuzitengea | C. kuitenga | D. kuwatengea |
| 9. | A. naye | B. nawe | C. nao | D. nayo |
| 10. | A. usoni | B. kisogoni | C. mwambo | D. karibuni |

Maishani yangu shuleni __11__ ya kupanda na kushuka. Zipo nyakati __12__ tulipewa adhabu kalikali __13__ tulipokosa kukamilisha mazoezi __14__ na walimu wetu. Hatimaye niliamua kufuata mawaidha niji nikaangamia baadaye kwani __15__.

- | | | | | |
|-----|---------------------------------------|---------------|---------------|---------------|
| 11. | A. ilikuwa | B. kulikuwa | C. yangukuwa | D. yalikuwa |
| 12. | A. ambazo | B. ambao | C. ambayo | D. ambalo |
| 13. | A. kamwe | B. abadan | C. hasa | D. jinsi |
| 14. | A. tuliopewa | B. tuliyopewa | C. tulilopewa | D. tulizopewa |
| 15. | A. baada ya dhiki ni faraja | | | |
| | B. asiyekubali kushindwa si mshindani | | | |
| | C. asiyesikia la mkuu huvunjika guu | | | |
| | D. mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo | | | |

Kutoka swali la 16 hadi 30 jibu kulingana na maagizo.

16. Ni maamkizi yapi yaliyoambatanishwa vyema?
A. U hali gani? - Mzuri
B. Sabalheri? - Masalheri
C. Cheichei? - Ewaa
D. Usiku mwaka? - Buriani
17. Neno mkeka lina silabi ngapi?
A. Tano
B. Nne
C. Mbili
D. Tatu
18. Tegua kitendawili kifuatacho
Kikigongwagongwa wanawe hutoka
A. kizimba
B. kichuguu
C. mzinga
D. chungu
19. Ni sentensi ipi iliyotumia kivumishi cha pekee?
A. Nyumba yoyote iliyojengwa pasipofaa itabomolewa
B. Wazazi wangu watasafiri kesho
C. Matunda mabivu yameliwa na watoto
D. Vitabu hivyo ndivyo vilivyosomwa
20. Nomino maradhi, mazingira na marashi zinapatikana katika ngeli gani?
A. U-U
B. LI-YA
C. YA -YA
D. I -I
21. Kanusha sentensi ifuatayo
Kujali kwangu kumenisaidia
A. Kujali kwangu hakujanisaidia
B. kutojali kwangu hakujanisaidia
C. kujali kwangu hakukunisaidia
D. kutojali kwangu hakutanisaidia
22. Andika kwa wingi
Sokwe amemla mkunga aliyevuliwa
A. Masokwe wamewala mikunga waliovuliwa
B. Sokwe wamewala wakunga waliovuliwa
C. Masokwe wameila mikunga iliyovuliwa
D. Sokwe wamewala mkunga waliovuliwa
23. Ni methali ipi yenye maelezo kuwa mtu anaposababisha shida huishia kuwahusisha watu wake au jamaa yake?
A. kikulacho ki nguoni mwako
B. msiba wa kujitakia hauna kilio
C. mchuma janga hula na wa kwao
D. mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe
24. Mtu anayehamia nchi nyingine na kufanya makao yake huko huitwa?
A. Mkimbizi
B. Mhaini
C. Balozi
D. Mlowezi
25. Ni alama ipi ya uakifishaji inayotumiwa kuonyesha orodha?
A. Ritifaa
B. Nukta mbili
C. Parandesi
D. Nukta na mkato

26. Ni sentensi ipi iliyotumia kiambishi ‘ki’ cha ngeli?
- A. Kiatu kilichoraruka kimeshonwa
 - B. Ukisoma kwa bidii utafua dafu
 - C. Kijibwa chake kinabweka
 - D. Mama alimenya viazi akiimba
27. Dada wa baba nitamwitaje?
- A. Halati
 - B. Mkoi
 - C. Ami
 - D. Shangazi
28. Tambua kivumishi katika sentensi ifuatayo
- Mwanafunzi mtiifu alituzwa jana
- A. alituzwa
 - B. mwanafunzi
 - C. mtiifu
 - D. jana
29. Ni kiungo kipi cha mwili kinachosafisha hewa?
- A. Ini
 - B. Pafu
 - C. Figo
 - D. Wengu
30. Kaidi ni fisi karamuni. Hii ni faini ipi ya lugha?
- A. Nahau
 - B. Tashbihi
 - C. Istiara
 - D. Tashihisi

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40.

Usiku mmoja katika kitongoji cha Tujihadhari, mvua ilinyesha kidindia ikiandamana na ngurumo za radi na umeme. Kwa kuwa mvua hiyo ilinyesha jioni, watu wote walilazimika kwenda kulala mapema kuliko ilivyokuwa hali yao ya kawaida.

Wavyele wangu walikuwa katika chumba chao, Mimi na ndugu yangu tulikuwa chumbani mwetu wakati mmuliko mmoja ulipopenya nyumbani mwetu, mkawa mweupe pe pe pe! kama ambamo mlikuwa taa ya umeme. Ghafla bin vuu, tulisikia mti mkubwa uliokuwa uani ukianguka kwa kishindo.

Pale barazani tulisikia kitu kikichugachuga gizani. Hatukuweza kutuhumu vyema kitu hicho kilikuwa nini au alikuwa mnyama yupi. Kwa ajili ya wasiwasi uliotupata, mimi na ndugu yangu tulijitupa vitandani na kujifunika mablanketi kutoka nyayoni hadi utosini.

Asubuhi kulipokucha , mvua ilikuwa imepusa na hali ya hewa ilikuwa shwari. Wakati huo mimi nilikuwa macho. Nilienda kufungua mlango huku mwili wangu ukisisimka kwa yale tuliyoyasikia usiku uliopita. Mara nilipofungua mlango nilimwona mnyama mkubwa amekingama mlangoni. Moyo ulidunda mithili ya ngoma na mkwiro kilingeni.

Mnyama huyo alikuwa na hatamu na saruji. Hapa ndipo nilipong'amua kwamba mnyama mwenyewe alikuwa farasi, Macho yalikuwa yamemtoka pima kama nanigwanzula aliye banwa mlangoni. Nilipoangaza macho zaidi nilikutana ana kwa ana na maiti ya binadamu . Nilipomkaribia zaidi na kumtazama kwa makini niliona kuwa maiti hiyo ilikuwa amekatwa vipande viwili kama kwamba ilikatwa kwa msumeno.

Nilitambua kuwa maiti hiyo ndiyo iliyokuwa ya mwenye farasi. Huenda alikuwa akija kwetu kujibari mvua na kuhepa dhoruba hiyo ya usiku uliotangulia. Kumbe alipigwa na radi tuliyoisikia na akawa amesafirishwa jongomeo pamoja na farasi wake. Lilikuwa ni tukio la kuhuzunisha ambalo lilituacha tukiwa tumepigwa na butwaa. Hakika wahenga hawakukosea waliponena kuwa ajali haina kinga wala kafara.

31. Kulingana na taarifa ni kweli kuwa____
 A. mvua iliwafanya baadhi ya watu kulala mapema
 B. mvua iliyonyesha iliandamana na radi pekee
 C. mvua ilinyesha kwa muda mrefu
 D. ilikuwa kawaida ya wakazi wa Tujihadhari kulala mapema
32. Kwa mujibu wa aya ya pili, si kweli kuwa
 A. hamkuwa na taa ya umeme katika chumba cha kulala.
 B. mmuliko wa umeme ulipenyeza vyumbani
 C. mti ulianguka uani baada ya mmuliko wa umeme
 D. mwandishi na wavyele wake walikuwa wamelala katika chumba kimoja
33.mkawa mweupe pepepe! Hii ni fani gani ya lugha?
 A. Tanakali ya sauti
 B. Tashbihi
 C. Istiara
 D. Nahau
34. Mwandishi na nduguye waliposikia kitu kikichugachuga_____
 A. walifahamu kuwa alikuwa ni farasi aliyegongwa na radi
 B. walielewa ni mti mkubwa ulionguka kutokana na radi
 C. hawakufahamu yaliyokuwa yakiendelea nje
 D. aliufungua mlango ili kujua kilichokuwa kikiendelea
35. Kwa nini mwandishi na ndugu yake walijifunika kwa mablanketi?
 A. Walijawa na ujasiri mwingi
 B. Kimuyemuye kilikuwa kimewakumba
 C. Walikuwa na usingizi kupita kiasi
 D. Walijawa na huzuni nyingi
36. Wakati wa asubuhi ulipowadia
 A. mvua ilikuwa imesimama na hali ya hewa kuwa tulivu
 B. hali ya hewa ilivurugika na mvua kupungua
 C. mvua ilipungua na hali ya hewa kwenda mrama
 D. mvua ilinyesha ya rasharasha na hali ya hewa kuwa shwari
37. Ni nini maana ya nilikuwa macho kulingana na taarifa?
 A. Niliogopa
 B. Nilijasirika
 C. Nilijihadhari
 D. Nilijibidiisha
38. Pindi mwandishi alipofungua mlango , alikutana na nini?
 A. Binadamu aliyekingama mlangoni akiwa mahututi
 B. Mti mkubwa ulioangushwa usiku uliotangulia
 C. Farasi aliyekuwa hai akiwa ameala mlangoni
 D. Mnyama aliyelala kutoka upande mmoja hadi mwingine.
39. Unafikiria ni nini kilichosababisha kifo cha mwenye farasi
 A. Mvua kubwa iliyomnyeshea
 B. Mngurumo wa radi na umeme
 C. Huenda farasi wake alimwangusha na kufa
 D. Alikatwa kwa msumeno na majambazi
40. Kichwa kinachofaa habari uliyoisoma ni kipi?
 A. Mvua iliyoleta balaa
 B. Usiku wa fanaka
 C. Siku iliyojaa wasiwasi
 D. Mvua yenye baraka na karaha

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.

Ufisadi ni tatizo ambalo limekuwa sugu katika nchi yetu ya Kenya. Kila mja anafahamu kama kitengele cha mkono wake kwamba upokeaji au utoaji wa chochote chenye thamani ili kupokea mapendeleo fulani ni hongo. Mara nyingi vyombo vya dola hujitia hamnazo huku sekta nyingi zikiendelea kuzama zii katika lindi hili hatari. Swali ni je, ni nani atainusuru nchi hii kutoka kwenye jinywa hili pana la ngwena?

Kila kunapokucha sakata ngeni huzuka mithili ya mizuka. Wanaohusika kama ilivyo desturi ni wenye uwezo pengine wakiwa ndani ya serikali au waliopokea umaarufu wao kwa mlango wa nyuma. Aidha, makabaila wanaoshiriki ukiritimba wako kwenye jedwali hili la kufyonza nchi hii rasilimali zake aali. Jambo hili limetufanya kuwa wadeni wa mataifa yaliyoendelea .

Kesi nyingi za uporaji hazijulikani zinavyoisha. Mara uidhinishaji wa kandarasi gushi, mara mikopo ya kigeni inayoishia mifuko ya wachache na hata safari zisizo na maana za wafanyakazi wa umma. Yote haya hurudi kwa walalahoi. Wao ndio hushikwa koo katika kugharamia.

Sheria za kuinua viwango vya mikopo ya nchi yetu kutoka nje hupitishwa bila ya hata hiari ya Wakenya. Wananchi husikia baadaye kuhusu madeni chunguchungu yanayodaiwa nchi yao na mataifa ya kigeni Jambo hili huwaacha wengi wakipigwa na butaa na kujiuliza maswali mengi yasiyo na majibu. Ama kweli wahenga hawakukosea waliponena kuwa mnyonge mnyongeni ama ukipenda mnyonge msonge.

Wengi mitaani wanaomba viongozi wetu waweze kuwajibika na kujitwika jukumu la kuilinda rasilimali yetu. Wawe kielelezo bora cha kuigwa na wengine hasa watoto wetu ambao ndio viongozi wa siku za halafu. Ni dhima ya kila mmoja wetu kusimama kidete na kupigana na nduli huyu. Sote tulivalie njuga suala hili na kuwakemea mafisadi kwa kinywa kipana. Wanaoshiriki ufisadi wafunguliwe mashataka na kupewa hukumu kali. Pamoja tuungane kuupiga ufisadi.

41. Ni nini maana ya maneno ufisadi ni tatizo ambalo limekuwa sugu kulingana na habari?
 A. Ufisadi ni jambo muhimu nchini
 B. Ufisadi umeweza kuangamizwa nchini
 C. Ufisadi hauwezi kuondolewa kwa urahisi
 D. Ufisadi ni jambo la thamani taifani
42. Kulingana na habari ufisadi umeelezwa kuwa ni nini?
 A. Utoaji na upokeaji wa kitu kwa njia ya halali.
 B. Hali ya mtu kujifikiria na kujipenda mwenyewe.
 C. Utoaji wa kitu cha thamani kwa manufaa ya wenine.
 D. Utoaji na upokeaji wa kitu chochote ili kufanyiwa mapendeleo.
43. Ni neno lipi ambalo haliwezi kutumiwa badala ya hongo?
 A. Chai
 B. Kiangaza macho
 C. Kiinikizo
 D. Mvugulio
44. ... sakata ngeni huzuka mithili ya mizuka. Hii ni fani gani ya lugha?
 A. Tashbihi
 B. Nahau
 C. Tashihisi
 D. Istiara
45. Wanaofuja rasilimali ya nchi si pamoja na _____
 A. mabwanyenye na wakiritimba
 B. makabaila na viongozi
 C. viongozi na mabwanyenye
 D. wakata na walalahoi
46. Kwa mujibu wa habari wadeni ni akina nani?
 A. Watu wanaotaka kupigwa jeki na wengine
 B. Watu wanaodaiwa na watu wengine
 C. Watu wanaotumia vyeo vyao ili kujinufaisha
 D. Watu wanaotaka kurejeshewa vitu vilivyo vyao
47. Ni kesi ipi ambayo haijatajwa inayohusiana na uporaji wa mali ya umma?
 A. Mikopo ya kigeni iliyotumiwa vibaya
 B. Kuidhinisha kandarasi gushi
 C. Utumiaji wa mikopo na mali ya umma kwa njia ya halali
 D. Safari zisizo na manufaa za wafanyakazi wa umma.
48. Ni nini maana ya wakipigwa na butaa kulingana na habari?
 A. Wakiwa na huzunia nyingi
 B. Wakiachwa na fedheha kubwa
 C. Wakisalia na mshangao mkubwa
 D. Wakiwa wenye hasira nyingi
49. Kulingana na aya ya mwisho ni kweli kusema kuwa:-
 A. Wengi wa wananchi wanaomba viongozi kutelekeza wajibu wao
 B. Ni jukumu la serikali pekee kupigana na ufisadi
 C. Watoto ni lazima wawe kielelezo cha kuigwa
 D. Kupitia ushirikiano, tutaweza kupigana na uovu huu
50. Ni methali ipi isiyofaa kulingana na aya ya mwisho, sentensi ya mwisho?
 A. Wapishi wengi hugaribu mchuzi
 B. Ukuni mmoja moto hauwaki
 C. Wawili si mmoja
 D. Nia zikiwa moja kilicho mbali huja.